# TOKENI MIJINI

E. G. White

Msaada kwa Maadili na Usalama wa

Jamii

Mkusanyo wa Maandiko

ya

ELLEN G. WHITE

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Country Living - Kiswahili

# DIBAJI

Faida za kuishi shamba [vijijini] zimesisitizwa tena na tena katika mashauri yanayotolewa na Roho ya Unabii. Mawingu ya dhoruba yanayojikusanya yanaashiria kwamba yafaa kuanza kupaza sauti ili kutoa wito wa kuihama miji. Ni budi iwe wazi kwa kila Mwadventista Msabato mwenye akili kujua ya kwamba kuishi mjini, pamoja na msongamano wa watu uliopo, vishawishi vyake na migogoro ya vyama vya wafanyakazi inayozidi kuongezeka, hakuweki mazingira yenye kuleta afya kwa familia za Kikristo.

Kwa miaka mingi maelfu ya Waadventista Wasabato wameelekezwa kuchagua mazingira yanayofaa kuweka makazi yao na katika uhusiano wao na mashirika ya ulimwengu kwa njia ya mashauri yatokanayo na shuhuda juu ya mambo hayo ya maana sana ambayo yamechapishwa na kutawanywa katika sehemu nyingi. Ishara mbaya za hatari kubwa iliyo karibu sana kutokea zinapoonyesha ugumu wa kuzitambua hatari hizo na ukali mno wa pambano lililo mbele yetu, inaonekana kwetu ya kwamba ni jambo linalofaa kuuchapisha tena ushauri huu kwa kutumia mtindo huu ambao unaweza kuyanasa mawazo ya kila mshiriki wa kanisa.

Na kwa kufikiria nyakati hizi tulizo nazo [hivi sasa], ni mahali pake, sio tu kurudia ushauri ule unaofahamika sana uliochapishwa muda mrefu uliopita, bali kuzitilia nguvu semi hizo kwa kuzitoa kwa mafundisho ya kinagaubaga yaliyopata kuchapishwa toka wakati hata wakati katika gazeti la Review and Herald au yaliyoandikwa katika barua zake za ushauri zilizoandikwa kwa watenda kazi waliokabidhiwa madaraka katika kazi ya Mungu. Kitendo kama hicho kinapatana kabisa na maagizo ya Bibi E. G. White kwa wadhamini wake ili waweze kutayarisha "kwa ajili ya kuchapishwa maandiko yangu yaliyokusanywa pamoja kutoka katika maandiko yangu ya mkono," kwa maana, kama alivyosema yeye mwenyewe yana "maagizo aliyonipa Bwana kwa ajili ya watu wake." Mwaka wa kuandikwa au kuchapishwa kwa mara ya kwanza umetolewa pamoja na kumbukumbu ya chanzo cha kila kifungu cha maneno [kilichotumika].

Wito wa dhati uliotolewa katika kijitabu hiki unataka pawepo na nia ya kutekeleza jambo hili, lakini [kwa wakati uo huo] onyo hili zito linatolewa ili watu wetu wasithubutu kukurupuka [kufanya mambo bila kufikiri na kupanga vizuri]. Tungependa kuyaelekeza mawazo yenu hasa kwa tahadhari zile zinazopatikana katika Sehemu ya Saba, "Kuongozwa kwa Maongozi ya Mungu," ambayo inatokea kwenye kurasa za . Kijitabu hiki sasa kinawekwa uwanjani kama jibu la msimamo ulioamuliwa na viongozi wa kanisa hili kwamba [sasa] wakati umefika wa kurudia kusema tena na tena kilio kile cha, "TOKENI MIJINI."

WADHAMINI WA UCHAPISHAJI WA MAANDIKO YA ELLEN G. WHITE

YALIYOMO

Ukurasa

Wito wa Kuihama Miji........................................................ ...........................

Kuikwepa Migogoro ya Vyama vya Wafanyakazi...............................................

Ombi kwa Wazazi........................................................ .....................................

Kazi Katika Sehemu za Shamba........................................................ .................

Kujiandaa kwa Hatari Itakayoletwa na Amri ya Jumapili....................................

Kujikusanya Watu Wengi katika Taasisi Zetu za Kazi.........................................

Kuongozwa kwa Maongozi ya Mungu........................................................ .......

Taasisi Zetu za Kazi Kuwa Mbali na Maeneo Yenye Msongamano wa Watu.......

SEHEMU YA KWANZA

Kukimbia Wakati wa Hali ya Hatari Pambano Litakapokuwa Linafikia Mwisho..

SEHEMU YA KWANZA

## Wito wa Kuihama Miji

### Hatari Kubwa Zilizomo Mijini

Ni wachache wanaotambua umuhimu wa kukwepa, kwa kadiri iwezekanavyo, uhusiano wo wote ule unaoleta uadui kwa maisha yetu ya kidini. Katika kuchagua mazingira yao, ni wachache mno wanaoweka mawazoni mwao ufanisi wao wa kiroho katika nafasi ya kwanza.

Wazazi na familia zao hukimbilia mijini, kwa sababu wanadhani kwamba ni rahisi kupata maisha mazuri huko kuliko mashambani [vijijini]. Watoto wao, wakiwa hawana kazi yo yote ya kufanya wasipokuwa shuleni kwao, hujipatia elimu ya mitaani. Kutoka kwa marafiki zao waovu wanajifunza tabia za uovu na ubadhirifu [utumiaji mbaya wa fedha na vitu]. Wazazi huyaona hayo yote, lakini itahitaji kujitolea mhanga kuweza kuyasahihisha makosa yao hayo, nao [wazazi] huendelea kuishi mahali hapo walipo mpaka Shetani anawatawala watoto wao kabisa.

Ni afadhali kujinyima mambo yote na kila tarajio la kidunia kuliko kuzihatirisha roho hizo za thamani mlizokabidhiwa kuzitunza. Watashambuliwa vikali na majaribu, nao yapasa wafundishwe jinsi ya kuyakabili; lakini ni wajibu wenu kuuondolea mbali kila mvuto, kulivunjilia mbali kila zoea, kukata kila kifungo kinachowazuia msiwe na uhuru kamili, ulio wazi, na kujitoa wakf ninyi wenyewe kwa moyo wenu wote pamoja na familia yenu kwa Mungu.

Badala ya msongamano wa watu uliomo mjini, tafuteni mahali fulani palipo kimya [pa upweke] kwa kadiri iwezekanavyo, mahali palipo salama mbali na majaribu, nanyi mkiwa pale waleeni na kuwaelimisha ili wapate kuwa watu wenye manufaa katika maisha yao. Nabii Ezekieli ndivyo anavyoorodhesha sababu zilizoifanya Sodoma kutenda dhambi na kuangamizwa: "Kiburi, chakula tele, na uvivu mwingi vilikuwa ndani yake pamoja na binti zake [vitongoji vyake]; wala haukuitia nguvu mikono ya maskini na wahitaji." Wale wote wanaotaka kuokoka ili wasipatikane na maangamizi kama yale ya Sodoma, hawana budi kuukwepa mwenendo ule ulioleta hukumu za Mungu juu ya mji ule mwovu." ----- Testimonies, Gombo la 5, uk. 232,233 (1882).

### Kuishi Mijini Sio Mpango wa Mungu

Ulimwenguni kote miji inageuka na kuwa mahali penye maovu mengi sana. Kila upande huonekana mambo machafu na sauti za uovu. Kila mahali kuna vishawishi vya kuamsha ashiki [tamaa mbaya ya uasherati] na ubadhirifu [matumizi mabaya ya mali na vitu]. Wimbi la rushwa na

uhalifu linazidi kuumuka daima. Kila siku inayopita huleta taarifa za kutumia nguvu ----- ujambazi, mauaji, kujiua, na uhalifu mwingine usiostahili hata kutajwa.

Maisha yaliyomo mijini sio maisha halisi, tena ni ya kinafiki. Tamaa kubwa sana ya kupata fedha, mambo ya mpwitompwito [msisimko] yapitayo kasi pamoja na kutafuta anasa, kiu ya kuwakoga [kujionyesha ufahari kwa] wengine, utajiri na ubadhirifu, mambo yote hayo ni nguvu ambazo, kwa sehemu kubwa sana ya wanadamu, huyageuzia mawazo yao mbali na kusudi halisi la maisha yao. Wanaufungua mlango wa kuingiza ndani yao maelfu ya maovu. Kwa vijana mambo hayo yana nguvu nyingi ambayo karibu haizuiliki kabisa.

Mojawapo ya majaribu yaliyojificha sana na ya hatari sana yanayowashambulia mno watoto na vijana katika miji ni kule kupenda anasa [starehe]. Sikukuu ni nyingi; michezo na mashindano ya mbio za farasi huwavuta maelfu, na ule mpwitompwito upitao upesi pamoja na anasa huwavuta kwenda mbali na majukumu mazito ya maisha yao. Fedha ambayo ingetunzwa kwa ajili ya kuitumia kwa mambo mazuri zaidi hutapanywa ovyo katika burudani zao nyingi.

Kutokana na utendaji wa mashirika ya amana, na matokeo ya vyama vya wafanya kazi na migomo yake, hali ya maisha mjini daima inakuwa ngumu zaidi na zaidi. Taabu kubwa ziko mbele yetu; na kwa familia nyingi kuondoka kwao kutoka mijini kutakuwa ni kwa lazima.

Mazingira ya nje katika miji mara nyingi ni ya hatari kubwa kwa afya. Uwezekano wa kudumu wa kupatwa na magonjwa, kuenea kwa hewa chafu, maji machafu, chakula kilichochafuliwa, majengo yaliyosongamana pamoja yenye giza na yasiyofaa kiafya, ni baadhi ya mambo mabaya ya kukabiliana nayo humo.

Halikuwa kusudi la Mungu kwamba watu waishi kwa kusongamana sana mijini, wakisongamana pamoja katika mlolongo wa majumba katika kitalu kimoja na katika nyumba za kupangisha zenye vyumba vingi. Hapo mwanzo aliwaweka wazazi wetu wale wa kwanza katikati ya madhari nzuri na sauti nzuri. Anataka sisi tuifurahie siku ya leo. Kadiri tunavyokaribia sana kuwa katika hali ile inayopatana na mpango wa Mungu wa awali, ndivyo kadiri tutakavyokuaa na nafasi nzuri zaidi ya kujipatia afya ya mwili, akili, na roho. ----- The Ministry of Healing, uk. 363-365. (1905)

## Moyo wa Kusitasita

Sikuweza kulala baada ya kupita saa nane ya usiku mpaka asubuhi ya leo. Wakati wa usiku nilikuwa natoa ushauri. Nilikuwa nazisihi baadhi ya familia kutumia njia alizoziweka Mungu, na kuondoka mijini ili kuwaokoa watoto wao. Wengine walikuwa wanasitasita tu, bila kufanya juhudi yo yote iliyo dhahiri.

Malaika wale wenye rehema walimharakisha Lutu na mkewe na binti zao kwa kuwashika mikono yao. Lutu angekuwa ameharakisha kama Mungu alivyotaka, mke wake asingegeuka na kuwa nguzo ya chumvi. Lutu alikuwa na roho hiyo ya kuchelewa-chelewa [kusitasita] mno. Hebu sisi na tusiwe

kama yeye. Sauti ile ile iliyomwonya Lutu kuondoka Sodoma inatuamuru sisi, ikisema, "Tokeni kati yao, mkatengwe nao... Msiguse kitu kilicho kichafu." [2 Kor. 6:17.] Wale wanaolitii onyo hilo watapata kimbilio. Hebu kila mwanaume na awe macho sana kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, tena ajaribu kuiokoa familia yake. Hebu na ajifunge kibwebwe [mkanda] kwa kazi hiyo. Mungu ataonyesha hatua kwa hatua linalopaswa kufanywa baada ya hapo.

Isikilizeni sauti ya Mungu kupitia kwa mtume wake Paulo, isemayo: "Utimizeni wokovu wenu kwa kutetemeka. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema" [Wafilipi 2:12,13]. Lutu akalikanyaga bonde lile tambarare kwa hatua za kujilazimisha na kuchelewa-chelewa tu. Kwa muda mrefu sana alikuwa amezoeana na watenda maovu wale hata hakuweza kuiona hatari kubwa iliyomkabili mpaka hapo mke wake aliposimama katika bonde lile akiwa nguzo ya chumvi milele." ----- Review and Herald, Des. 11, 1900.

## Miji Itapatilizwa kwa Hukumu za Mungu

Wakati umekaribia ambapo miji mikubwa itapatilizwa kwa hukumu za Mungu. Katika kitambo kidogo tu kilichobaki, miji hiyo itatikiswa vibaya mno. Haidhuru iwe mikubwa kiasi gani au majengo yake yawe imara jinsi gani, haidhuru vifaa vya kujihami na moto viwe vimeandaliwa kwa wingi namna gani, acha Mungu ayaguse majengo hayo, katika muda wa dakika chache tu au saa chache yatakuwa yameharibiwa kabisa na kuwa magofu.

Miji hiyo miovu [isiyomcha Mungu] itafagiliwa mbali kwa fagio la maangamizi. Katika uharibifu unaoyapata majengo makubwa na sehemu kubwa za miji hivi sasa, Mungu anatuonyesha kile kitakachoiangukia dunia yote. ----- Testimonies, Gombo la 7, uk. 82,83. (1902).

## Matokeo ya Maonyo Yaliyopuuzwa

Nimeagizwa kutangaza ujumbe huu kuwa miji ile iliyojaa maasi [uvunjaji wa sheria], na ile iliyo miovu kupita kiasi, itaharibiwa kwa matetemeko, kwa moto, na kwa mafuriko. Dunia yote itaonywa na kujua kwamba yuko Mungu atakayedhihirisha mamlaka yake kama Mungu. Mawakala [wajumbe] wake wasioonekana kwa macho [malaika] watasababisha maangamizi, kuteketeza kwa moto, na vifo. Utajiri wote uliolundikwa utakuwa kama si kitu....

Maafa yatakuja ----- yaani, maafa ya kuogofya mno, yasiyotarajiwa kabisa; na maangamizi hayo yatafuatana moja baada ya jingine. Kama watu watayasikia [watayatendea kazi] maonyo haya ambayo Mungu ametoa, na iwapo makanisa yatatubu, na kurudia utii wao [kwa Mungu], basi, miji mingine itaachwa isiharibiwe kwa muda fulani. Lakini endapo watu waliodanganyika wataendelea kutembea katika njia ile ile walimokuwa wakitembea, wakiendelea kuidharau Sheria ya Mungu [Amri Kumi], na kuhubiri [mafundisho ya] uongo mbele ya watu, basi, Mungu ataruhusu majanga yawapate ili akili zao zipate kuamshwa.

Bwana hatawatupilia mbali kwa ghafula wale wote wanaozivunja amri zake [kumi], wala kuyaangamiza mataifa mazima; lakini ataiadhibu miji na mahali pale ambapo watu wamejitoa kabisa kutawaliwa na nguvu za kishetani. Kwa ukali sana miji ya mataifa itashughulikiwa, hata hivyo haitapatilizwa kwa ghadhabu kali mno ya Mungu, kwa sababu baadhi ya watu waliomo humo watajinasua kutoka katika madanganyo hayo ya yule adui [Shetani], kisha watatubu na kuongolewa, na wakati uo huo watu wengi sana watakuwa wanajiwekea akiba ya ghadhabu kwa siku ile ya ghadhabu [ya Mwana-Kondoo, yaani, Kristo]. [Ufunuo 6:14-17; 15:1; 16:1-21.] ----- Evangelism, uk. 27. (1906)

## Ukaribu Sana wa Kuja kwa Hukumu za Mungu

Zipo sababu kwa nini sisi tusijenge [nyumba zetu] mijini. Juu ya miji hii, hukumu za Mungu zi karibu sana kuiangukia. ----- Letter 158, 1902.

Laiti kama watu wa Mungu wangeyajua maangamizi yaliyo karibu sana kuja juu ya maelfu ya miji, ambayo kwa sasa imejisalimisha kabisa kuabudu sanamu [Kol. 3:5,6; Efe. 5:5-7; Kut. 20:4-6]. ----- Review and Herald, Sept. 10, 1903.

## Maono ya Maangamizi Makubwa

Alfajiri Ijumaa iliyopita, kabla tu sijaamka usingizini, mandhari [picha] iliyonigusa sana moyoni ilionyeshwa mbele yangu. Nikajiona kana kwamba nimeamka usingizini, ila sikuwa nyumbani mwangu. Kupitia katika madirisha niliweza kuona moto mkubwa wa kutisha uliokuwa unayateketeza majumba. Mipira mikubwa ya moto [huenda ikawa ni mabomu] ilikuwa ikidondoka juu ya nyumba zile, na kutoka katika mipira hiyo mishale ya moto ilikuwa inaruka kuelekea kila upande. Ilikuwa haiwezekani kabisa kuizuia mioto hiyo iliyokuwa imewashwa, tena mahali pengi palikuwa panaharibiwa. Hofu kuu iliyowashika watu ilikuwa haielezeki. ----- Evangelism, uk. 29. (1900)

## Juhudi za Mungu za Kuwaamsha Watu

Nikiwa bado ningali pale Loma Linda, California, Aprili 16, 1906, maono ya ajabu sana yalipita mbele yangu. Wakati wa njozi zangu za usiku, nalikuwa nimesimama kwenye mwinuko [kilima], kutoka hapo niliweza kuziona nyumba zikitikiswa kama tete katika upepo. Majengo, makubwa kwa madogo, yalikuwa yakianguka chini. Majumba ya anasa wanayoyatembelea watu wengi, nyumba za michezo ya kuigiza, hoteli, na nyumba za matajiri zilitikiswa na kuharibiwa kabisa. Maisha mengi yakafutiliwa mbali, na anga ilikuwa imejaa sauti za vilio vikubwa kutokana na wale waliokuwa wamejeruhiwa na kuogofywa sana.

Malaika wa Mungu waangamizao walikuwa wanafanya kazi yao. Mguso mmoja tu, majengo yaliyojengwa imara sana ambayo watu walifikiri kwamba yalikuwa salama kutokana na hatari ya kila namna, kwa ghafula yakawa malundo ya takataka. Hapakuwa na hakika ya kuwa na usalama mahali po pote pale. Mimi sikujiona kuwa nimo katika hatari yo yote maalum, lakini utisho mkuu wa matukio yale yaliyopita mbele yangu mimi siwezi kupata maneno ya kuelezea. Ilionekana kana kwamba uvumilivu wa Mungu ulikuwa umefikia kikomo chake kabisa, na ya kwamba siku ile ya hukumu ilikuwa imekuja.

Malaika yule aliyekuwa amesimama kando yangu ndipo akanipasha habari kwamba ni wachache tu waliokuwa na wazo lo lote kuhusu uovu uliomo katika ulimwengu wetu hivi leo, na hasa uovu ule ulio katika miji mikubwa. Akatangaza kwamba utawala wa Mungu ulio mkuu kuliko wote, na utakatifu wa Sheria yake [Amri Kumi], havina budi kufunuliwa kwa wale wanaoendelea kukataa kutoa utii wao kwa Mfalme huyo wa wafalme. Wale wanaochagua kubaki katika hali yao ya uasi [kuvunja Amri zake Kumi], ni lazima wapatilizwe kwa hukumu kwa rehema [zake Mungu], ili, kama ikiwezekana, wapate kuamshwa [kuzinduliwa] watambue uovu wa njia yao. ----- Testimonies, Gombo la 9, uk. 92,93. (1909)

## Hatari Itakayowakabili Watakaoendelea Kubaki Mjini Bila Sababu

Kulingana na nuru ile niliyopewa, mimi nawasihi watu kutoka na kuvihama vituo vikubwa vilivyojaa watu wengi. Miji yetu inazidi kuwa miovu, tena, inaonekana wazi zaidi na zaidi ya kwamba wale watakaobaki ndani ya miji hiyo bila sababu [ulazima wo wote] watafanya hivyo kwa athari kubwa ya wokovu wa nafsi zao. ----- Manuscript 115, 1907.

SEHEMU YA PILI

## Kuikwepa Migogoro ya Kazi

### Ondokeni [Mijini] Kwenda Vijijini Kwenye Uhuru

Wakati unaharakisha sana kuja ambapo uongozi wa Vyama vya Wafanyakazi utatumia uwezo wake kuleta mateso mengi kwa watu. Tena na tena Bwana ameniagiza kwamba watu wetu watoke mijini pamoja na familia zao kwenda vijijini, ambako wanaweza kujipatia chakula chao wenyewe; kwa maana siku zijazo tatizo la kununua na kuuza litakuwa zito sana. Hivi sasa tungeanza kuyatii maagizo hayo yaliyotolewa kwetu tena na tena. Tokeni mijini kwenda kwenye maeneo ya shamba [vijijini], ambako nyumba hazijasongamana sana mahali pamoja, na ambako mtakuwa huru mbali na usumbufu utakaoletwa na wale adui zetu. ----- Letter 5, 1904.

### Iepukeni Migongano Iletwayo na Vyama

Watu wamejiunga katika mashirika yenye kusudi baya ili kumpinga Bwana wa majeshi. Mashirika hayo yenye kusudi baya yataendelea kuwapo mpaka hapo Kristo atakapoondoka mahali pake pa maombezi mbele ya kiti kile cha neema, na kuvaa mavazi yake ya kulipiza kisasi [Ufu. 19:11-16]. Mawakala [wajumbe] wa Shetani wamo katika kila mji, wanashughulika sana kuwakusanya katika vyama wale wote wanaoipinga Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Wale wanaodai kuwa ni watakatifu na wale wanaosema waziwazi kuwa wao ni waumini wanachagua na kusimama upande wa vyama hivyo. Huu sio wakati wa kuwa dhaifu kwa watu wa Mungu. Hatuwezi kumudu kukaa bila kukesha [kuwa macho] hata kwa dakika moja. ----- Testimonies, Gombo la 8, uk. 42. (1904).

### Dhiki Itakayoletwa na Vyama vya Matajiri I Mbele Yetu

Vyama vya Matajiri [Waajiri] vitakuwa ni njia mojawapo itakayoleta duniani wakati wa taabu ambao haujapata kuwako [kuonekana] tangu mwanzo wa dunia hii. ----- Letter 200, 1903.

## Migogoro Kati ya Mashirikisho ya Matajiri na Vyama vya Wafanyakazi

Kazi wanayopaswa kufanya watu wa Mungu ni kujiandaa kwa matukio yale ya siku zijazo, ambayo yatawajia ghafula kwa nguvu nyingi. Ulimwenguni humu mashirika makubwa sana yenye ukiritimba [yanayomiliki na kuhodhi mali nyingi] yataundwa. Watu watajifunga wenyewe kwa mikataba katika vyama mbalimbali ambavyo vitawafungia katika mazizi ya yule adui. Watu wachache watajiunga pamoja na kuishika kwa nguvu mali yote iliyopatikana katika mikondo fulani ya biashara. Vyama vya Matajiri [Waajiri] vitaundwa, na wale wote wanaokataa kujiunga na vyama hivyo watakuwa watu wanaoangaliwa kwa jicho baya sana. ----- Letter 26, 1903.

## Kujiandaa kwa Tukio Hilo

Vyama vya Matajiri na mashirikisho ya ulimwengu huu yenye kusudi baya ni mtego kwetu. Achana nayo, na kwenda mbali nayo, enyi ndugu zangu. Msishirikiane nayo kabisa. Kwa sababu kwa ajili ya vyama hivyo na mashirikisho hayo yenye kusudi baya, muda si mrefu itakuwa vigumu sana kwa taasisi zetu kutekeleza kazi zake mijini. Onyo langu ni hili: Ondokeni mijini. Msijenge hospitali zetu zo zote mijini. Waelimisheni watu wetu watoke mijini kwenda mashambani [vijijini], ambako wataweza kujipatia sehemu ndogo ya ardhi, na kujijengea makazi yao wenyewe pamoja na watoto wao....

Migahawa yetu haina budi kuwekwa mijini; maana vinginevyo watumishi wa migahawa hiyo wasingeweza kuwafikia watu na kuwafundisha kanuni za maisha bora. Na kwa wakati huu tutakalia nyumba za mikutano [makanisa] zilizomo mijini. Lakini kabla ya muda mrefu kupita kutakuwa na vita na machafuko mijini ya aina ambayo wale watakaotamani kuihama [miji] hawataweza kufanya hivyo. Yatupasa tuwe tunajiandaa [sasa] kukabiliana na matatizo hayo. Hii ndiyo nuru niliyopewa mimi. ----- General Conference Bulletin, Aprili 6, 1903.

## Kuuhifadhi Utu Wetu

Kwa miaka mingi nimepewa nuru ya pekee kwamba hatupaswi kuweka makao makuu ya kazi yetu mijini. Misukosuko na machafuko yanayoijaza miji hiyo, hali zile zitakazoletwa na Vyama vya Wafanyakazi na migomo yao, itakuwa kizuizi kikubwa kwa kazi yetu. Watu wanajaribu kuwafunga chini ya vyama fulani wale wote wanaofanya kazi mbalimbali. Huo sio mpango wa Mungu, bali ni

mpango wa mamlaka ambayo kwa vyo vyote vile tusingekubaliana nayo. Neno la Mungu linaendelea kutimia; waovu wanajifunga wenyewe katika matita matita tayari kuchomwa moto.

Hivi sasa yatupasa kutumia uwezo wote tuliopewa [na Mungu] katika kuutoa ujumbe wa onyo la mwisho kwa ulimwengu mzima. Katika kazi hii hatuna budi kuuhifadhi utu wetu. Hatupaswi kujiunga na vyama vya siri au na vyama vya matajiri na vya wafanyakazi. Tunatakiwa kusimama huru ndani ya Mungu, daima tukiwa tunamtazama Kristo kwa maagizo yake. Kuhama kwetu kote kutoka mahali fulani kwenda mahali pengine kufanyike kwa kuzingatia umuhimu wa kazi inayotakiwa kutimizwa kwa ajili ya Mungu wetu. ----- Testimonies, Gombo la 7, uk. 84. (1902)

## Kuidharau Sheria ile ya Amri Kumi

Vyama hivyo ni mojawapo ya dalili za siku za mwisho [Yakobo 5:1-6]. Watu wanajifunga wenyewe katika matita matita tayari kuchomwa moto. Pengine hao ni washiriki wa kanisa, lakini wanapojiunga na vyama hivyo, hakuna uwezekano kwao wa kutunza amri [kumi] za Mungu; kwa maana kule kujiunga na vyama hivyo maana yake ni kuidharau kabisa Sheria ile ya Amri Kumi.

"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako" [Luka 10:27]. Maneno hayo yanaweka jumla ya wajibu wote umpasao mwanadamu. Yana maana ya kuutoa wakf mwili wote, yaani, mwili, roho, na nafsi, kwa kazi ya Mungu. Watu wanawezaje kuyatii maneno hayo, na wakati uo huo kujifunga wenyewe kwa kiapo cha kukisaidia [chama] kile kinachowanyima uhuru wa kufanya mambo yao majirani zao? Tena, inawezekanaje kwa watu kuyatii maneno hayo, na kuyaunda mashirika yanayowadhulumu watu maskini haki zao ambazo wanastahili kupata, yakiwazuia wasinunue wala wasiuze isipokuwa kwa masharti fulani yaliyowekwa? ----- Letter 26, 1903.

## Vyama Vinavyoundwa au Vile Vitakavyoundwa

Wale wanaodai kuwa ni watoto wa Mungu kwa vyo vyote vile hawatakiwi kujifungamanisha na vyama vya wafanyakazi vinavyoundwa au vile vitakavyoundwa [baadaye]. Jambo hilo Bwana anakataza. Je! wale wanaojifunza unabii hawawezi kuona na kuelewa yale yaliyo mbele yetu? ----- Letter 201, 1902.

## SEHEMU YA TATU

### Ombi Kwa Wazazi

### Waondoeni Watoto Wenu Mbali na Mahali Penye Maovu

Faida yo yote ipatikanayo kutokana na shughuli za kila siku za maisha haya isiruhusiwe kuwashawishi wazazi kuacha kuwalea watoto wao. Kila inapowezekana, ni wajibu wa wazazi kujenga makao yao mashambani [vijijini] kwa ajili ya watoto wao. Watoto na vijana wanapaswa kulindwa kwa uangalifu. Wangeondolewa na kupelekwa mbali na mahali penye maovu mengi ambapo panapatikana katika miji yetu. Hebu na wazungushiwe mivuto ile inayopatikana katika nyumba ya kweli ya Kikristo ----- yaani, nyumba ile anamokaa Kristo. ----- Letter 268, 1906.

### Kabla Pigo Lile Halijafurika

Kabla pigo lile halijafurika juu ya wakazi wa dunia hii, Bwana anawaagiza wale walio Waisraeli kweli kweli kujiweka tayari kwa tukio lile. Kwa wazazi anawapelekea kilio cha onyo, akisema, Wakusanyeni watoto wenu na kuwaleta nyumbani mwenu; wakusanyeni na kuwatenga mbali na wale wanaozidharau amri [kumi] za Mungu, yaani, wale wanaofundisha watu uovu na kutenda uovu. Tokeni nje ya miji mikubwa haraka iwezekanavyo. Jengeni shule zinazoendeshwa na kanisa.

Wapeni watoto wenu Neno la Mungu kama msingi wa elimu yao yote. ----- Testimonies, Gombo la 6, uk. 195.

Nimeagizwa na Bwana niwaonye watu wetu wasikimbilie kwa wingi mijini ili kujijengea makazi humo kwa ajili ya familia zao. Kwa akina baba na akina mama nimeagizwa kusema maneno haya, Msikose kuwatunza watoto wenu ili wabaki ndani ya maeneo ya nyumba na viwanja vyenu. ----- Manuscript 81, 1900.

## Roho za Watoto Wenu au Maisha Rahisi na Starehe Zenu

Ninyi msiendelee tena kuwaweka watoto wenu mahali pale watakapokabiliana na majaribu yaliyomo mijini, miji ambayo imefikia kilele chake cha kuangamizwa. Bwana ametuma onyo lake kwetu pamoja na ushauri wake ili tutoke mijini. Basi na tusiendelee kuweka vitega uchumi zaidi katika miji hiyo. Akina baba na mama, mnazifikiriaje roho za watoto wenu? Je! mnawatayarisha waliomo nyumbani mwenu kwa kunyakuliwa kwenda katika majumba yale ya kifalme kule mbinguni? Je! mnawaandaa hao kuwa miongoni mwa familia ile ya kifalme? yaani, watoto wa Mfalme yule wa mbinguni? "Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake?" [Mathayo 16:26.] Mtalinganishaje maisha rahisi, starehe,hali ile yenye manufaa isiyo na wasiwasi [iliyomo humo mijini] na thamani ya roho za watoto wenu? ----- Manuscript 76, 1905.

## Tabia za Kikristo Zinajengeka Vizuri Zaidi Katika Maeneo ya Upweke

Hakuna hata familia moja katika mia ambayo ikiendelea kukaa mjini itakuwa na maendeleo mazuri kimwili, kiakili, au kiroho. Imani, tumaini, upendo, furaha, vinaweza kupatikana kwa vizuri zaidi katika mahali pa upweke, ambapo pana mashamba na vilima na miti. Nendeni na watoto wenu mbali na mambo yale yanayoonekana waziwazi [tamasha] na sauti za mjini, mbali na makelele ya magari yanayopita mitaani pamoja na makundi ya watu, hapo ndipo akili zao [watoto wenu] zitakuwa na afya zaidi. Itaonekana kuwa ni rahisi zaidi kwao kuikumbuka mioyoni mwao kweli ile ya Neno la Mungu. ----- Manuscript 76, 1905.

Wapelekeni watoto wenu kwenye shule zile zilizomo mjini, ambako kila aina ya majaribu huwangojea ili kuwatamanisha na kuwadhalilisha, ndipo kazi ile ya kujenga tabia itakuwa ngumu mara kumi kwa pande zote mbili, yaani, kwa wazazi na kwa watoto. ----- Fundamentals of Christian Education, uk. 326. (1894)

## Kimbilio Katika Maeneo ya Mashambani

Wazazi na waelewe ya kwamba malezi ya watoto wao ni kazi ya maana katika kuziokoa roho zao. Katika maeneo yale ya mashambani [vijijini] mazoezi ya viungo mengi ya kufanya yenye manufaa [kiafya] yatapatikana kwa kufanya mambo yale yanayopaswa kufanywa, ambayo yatawapa afya ya kimwili kwa kuzikuza neva zao na misuli. Tokeni mijini, huo ndio ujumbe wangu kwa ajili ya kuwalea watoto wetu katika maadili mema.

Mungu aliwapa wazazi wetu wale wa kwanza njia ya elimu ya kweli alipowaagiza kuilima ardhi na kuyatunza makao yao katika Bustani ile. Baada ya dhambi kuingia, kutokana na utovu wao wa utii kwa matakwa yake Bwana, kazi iliyofanyika kuilima ardhi ikawa imeongezeka sana, maana nchi, kutokana na laana ile, ikazaa magugu na michongoma. Lakini kazi ile yenyewe haikutolewa kwao kwa sababu ya dhambi. Bwana Mkuu Mwenyewe akaibarikia kazi ile ya kuilima ardhi.

## "KAMA VILE ILIVYOKUWA ... SIKU ZA NUHU"

Ni kusudi lake Shetani kuwashawishi wanaume na wanawake kwenda mijini, isitoshe, ili kufikia lengo lake anavumbua kila namna ya mambo mapya [mitindo mipya] na burudani, kila aina ya mambo ya kusisimua. Na miji ya ulimwengu wa leo inageuka na kuwa kama ilivyokuwa miji ile kabla ya Gharika.

Daima tungebeba mzigo huo [wa kujihadhari] tunapoyaona maneno hayo ya Kristo yakitimia, "Kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." Mathayo 24:37. Katika siku zile kabla ya Gharika, kila aina ya burudani ilibuniwa ili kuwafanya wanaume na wanawake kuwa na usahaulifu [wa mambo ya Mungu] na kutenda dhambi. Leo hii, mwaka huu wa 1908, Shetani anafanya kazi yake kwa nguvu nyingi, ili hali zile zile zipate kuwapo. Nao ulimwengu unazidi kuwa mwovu. Uhuru wa dini hautaheshimiwa sana na wale wanaojiita Wakristo, kwa kuwa wengi wao hawayajui kabisa mambo ya kiroho.

Hatuwezi kushindwa kuona ya kwamba mwisho wa ulimwengu huu karibu sana unakuja. Shetani anafanya kazi yake katika mioyo [mawazo] ya wanaume na wanawake, na wengi wanaonekana kana kwamba wamejazwa na tamaa ya kupata burudani na misisimko. Kama vile ilivyokuwa katika siku zile za Nuhu, kila aina ya uovu inazidi kuongezeka. Kwa wakati kama huu, watu wale

wanaojaribu kuzishika amri [kumi] za Mungu wangetafuta mahali pa upweke [pa kuishi] mbali na miji hiyo....

## SI HASARA KWENU

Ni nani basi atakayeonywa? Tunarudia tena kusema, Tokeni Mijini. Msidhani kwamba ni hasara kubwa sana kwenu, kwamba ni lazima kwenda vilimani na milimani, bali tafuteni mahali pale pa upweke [ukimya] ambapo mnaweza kuwa na Mungu peke yenu, mkijifunza mapenzi yake na njia yake....

Ninawasihi watu wetu kuifanya iwe ndiyo kazi yao ya maisha kutafuta maisha yao ya kiroho. Kristo yu mlangoni. Hii ndiyo maana nawaambia watu wetu, Msifikirie ya kuwa ni taabu mnapoitwa kuiacha miji na kuhamia katika maeneo ya shamba [vijijini]. Huko mibaraka mingi inawangojea wale watakaoishikilia. Kwa kuziangalia mandhari zile [sura za nchi] za maumbile, yaani, kazi ile ya Muumbaji, kwa kujifunza kazi ya mikono yake [uumbaji wake] Mungu, bila kujitambua mtabadilishwa na kufanana naye. ----- Manuscript 85, 1908.

## Kujipatia Matunda Bora Kabisa ya Maisha Haya

Jengo la gharama nyingi, fanicha iliyonakishiwa sana, mapambo, anasa, na raha, mambo hayo hayaleti hali zile zilizo za muhimu kwa maisha ya furaha, yenye manufaa. Yesu alikuja hapa duniani kufanya kazi kubwa sana iliyopata kufanywa miongoni mwa wanadamu. Alikuja kama balozi [mjumbe] wa Mungu, kutuonyesha sisi jinsi ya kuishi ili tuweze kujipatia matunda bora kabisa ya maisha haya. Ni hali [mazingira] gani basi zilizochaguliwa na Baba yetu wa milele kwa ajili ya Mwanawe? Ni nyumba ile iliyokaa mahali pale pa upweke [kimya] katika vilima vile vya Galilaya; nyumba iliyopata mahitaji yake kwa kazi ya uaminifu, yenye heshima; maisha yale ya kawaida; kupambana kila siku na matatizo pamoja na shida; kujikana nafsi, matumizi mazuri ya kipato chao, na huduma yao iliyotolewa kwa moyo wa uvumilivu na furaha; saa ile ya kujifunza kando ya mama yake, wakiwa na gombo la Maandiko lililofunguliwa wazi; macheo yale tulivu au utusitusi ule wa asubuhi katika bonde lile la majani mabichi; huduma takatifu ya maumbile yale; kujifunza uumbaji na maongozi ya Mungu; na moyo wake kuwasiliana na Mungu, ----- hizo zilikuwa ndizo hali [mazingira] na nafasi nzuri za maisha ya mwanzo ya Yesu.

## WAKUU NI URITHI UTOKANAO NA MAISHA YA SHAMBA

Hivyo ndivyo ilivyo kwa sehemu kubwa ya watu walio bora na wakuu katika vizazi vyote. Someni historia ya Ibrahimu, Yakobo, na Yusufu, na ya Musa, Daudi, na Elisha. Jifunzeni maisha ya watu wa nyakati zilizofuata baadaye waliostahili kabisa kuzijaza nafasi zile za amana na madaraka, watu ambao mvuto wao umekuwa na mafanikio makubwa sana katika kuuinua juu ulimwengu huu.

Ni wangapi miongoni mwa hao walilelewa katika makazi ya mashambani [vijijini]. Hawakuijua anasa hata kidogo. Hawakuutumia ujana wao katika burudani. Wengi walilazimika kupigana na umaskini na shida. Walijifunza mapema kufanya kazi [kwa mikono yao], na maisha yao ya kujishughulisha sana katika maeneo yale yaliyo wazi yaliwapa nguvu za kimwili na kupanuka kwa uwezo wao kiakili. Wakiwa wamelazimika kutegemea rasilimali [nyenzo] zile walizokuwa nazo, walijifunza kupambana na shida na kuvishinda vipingamizi, tena walijipatia ujasiri na uvumilivu. Walijifunza masomo ya kujitegemea na kujitawala nafsi zao. Wakiwa wamekingwa kwa kiwango kikubwa mbali na marafiki wabaya, walitosheka na furaha za kawaida na urafiki mzuri ujengao. Katika uchu wao wa chakula walifuata chakula cha kawaida na kuwa na kiasi katika mazoea yao. Walitawaliwa na kanuni, tena walikua wakiwa safi [wakiwa na mwenendo mzuri], wakiwa na nguvu na unyofu wa moyo. Walipotakiwa kufanya kazi zao za maisha, walikwenda wakiwa na nguvu za kimwili na kiakili, wakiwa na moyo uliochangamka, na uwezo wa kupanga mipango na kuitekeleza, tena wakiwa na uthabiti wa kuyapinga maovu, mambo ambayo yaliwafanya kuwa na uwezo dhahiri wa kutenda mema ulimwenguni.

## BORA KULIKO UTAJIRI

Bora kuliko urithi mwingine wo wote mnaoweza kuwapa watoto wenu itakuwa ni zawadi ile mtakayowapa ya mwili wenye afya, akili timamu, na tabia nzuri. Wale wanaojua kile kinacholeta ufanisi wa kweli katika maisha haya mara nyingine watakuwa na busara. Wataweka mbele yao mambo yale yaliyo bora kwa namna watakavyochagua makazi yao.

Badala ya kuishi mahali pale ambapo kazi za wanadamu zinaweza kuonekana waziwazi, penye tamasha na sauti zinazoamsha mawazo machafu, mahali pale ambapo misukosuko na ghasia huleta uchovu na wasiwasi, nendeni mahali ambako mnaweza kuangalia kazi za [uumbaji wa] Mungu. Jipatieni pumziko la nafsi zenu katika uzuri na utulivu na amani ya maumbile [viumbe vya asili]. Jicho lenu na liangalie mashamba ya chanikiwiti, vijisitu, pamoja na vilima. Angalieni mbingu ile ya samawi, isiyozuiwa na vumbi na moshi wa mjini hata isiweze kuonekana, vuteni hewa ile ya mbinguni inayowatia nguvu. Mbali na mambo yale yaliyomo mjini yanayovuta mawazo yenu na kuyatawanya, nendeni pale mnapoweza kukaa kirafiki na watoto wenu, mnapoweza kuwafundisha ili wapate kujifunza habari za Mungu kwa njia ya kazi zake [uumbaji wake], na kuwalea ili wawe na maisha ya unyofu na yenye manufaa [kwao wenyewe na kwa wengine]. ----- The Ministry of Healing, uk. 265-267. (1905)

## Faida Nyingi za Shughuli Zinazofanyika Nje

Lingekuwa ni jambo jema kwenu kuweka kando masumbufu yenu yanayowafadhaisha, na kupata mahali pa faragha huko shamba [vijijini], ambako hakuna mvuto wenye nguvu wa kuyaharibu maadili ya watoto na vijana wenu.

Ni kweli, hamtaweza kuondokana kabisa na maudhi yote pamoja na masumbufu yanayofadhaisha; lakini kule mgeweza kuyaepuka maovu mengi na kufunga mlango dhidi ya gharika ya majaribu yanayotishia kuyatawala kabisa mawazo ya watoto wenu. Wanahitaji kazi ya kufanya na mambo mbalimbali tofauti ya kushughulika nayo. Mambo ya jinsi ile ile waliyozoea kufanya nyumbani mwenu huwafanya wasiwe na raha [huwakinai], na kuwa watukutu, kisha wanajiingiza katika tabia ile ya kujichanganya pamoja na vijana wale waovu wa mjini, hivyo hujipatia elimu ya mitaani huko....

Kuishi huko shamba [vijijini] kungewaletea [watoto na vijana] manufaa mengi sana; maisha yao ya shughuli nyingi nje ya nyumba yangekuza afya yao kiakili na kimwili. Wawe na bustani ya kupalilia, ambamo watapata furaha na kazi yenye manufaa kwao. Kuitunza mimea na maua kuna mwelekeo wa kukuza akili za kupambanua mema na mabaya pamoja na kuwa na busara, na wakati uo huo ufahamu wao kuhusu uumbaji mzuri na wenye manufaa wa Mungu una mvuto kwao unaowabadilisha na kuwafanya wawe waungwana katika mawazo yao, wakiuhusisha [uumbaji huo] na Muumbaji na Bwana huyo wa vyote. ----- Testimonies, Gombo la 4, uk. 136. (1876)

## Tusitazamie Mwujiza Wo Wote Kuigeuza Njia Yetu Mbaya

Nayaangalia maua haya, na kila wakati ninapoyaangalia nafikiria juu ya Edeni. Hayo yanaonyesha upendo wa Mungu alio nao kwetu. Hivyo anatupatia sisi katika dunia hii mwonjo mdogo tu wa Edeni ile. Anatutaka sisi kufurahia vitu vizuri alivyoviumba, na ndani yake kuona sura [picha] ya kile anachotaka kutufanyia sisi.

Anatutaka sisi kuishi mahali pale palipo na nafasi tele. Watu wake hawatakiwi kusongamana mijini. Anawataka waende na familia zao nje ya miji, ili wapate kujiandaa vizuri kwa ajili ya uzima ule wa milele. Kitambo kidogo [kilichobaki] watalazimika kuondoka mijini.

Miji hiyo imejaa uovu wa kila namna, ----- pamoja na migomo na mauaji na watu kujiua wenyewe. Shetani yu ndani yake [miji hiyo], akiwaongoza watu katika kazi yao ya maangamizi. Chini ya mvuto wake wanaua kwa sababu tu ya kuua, na kitendo hicho wataendelea zaidi na zaidi kufanya....

Tukijiweka wenyewe chini ya mivuto ile mibaya iliyokatazwa, je! tutazamie kwamba Mungu atafanya mwujiza wo wote wa kuigeuza njia yetu hiyo mbaya? ----- La, hasha. Tokeni mijini haraka iwezekanavyo, na kununua sehemu ndogo ya ardhi [vijijini], ambako mnaweza kuwa na

bustani, mahali ambako watoto wenu wanaweza kuyaangalia maua yakuapo, na kujifunza kwayo mafunzo ya kuwa na maisha ya kawaida na usafi wa moyo. ----- General Conference Bulletin, Machi 30, 1903.

SEHEMU YA NNE

## Kazi Mbalimbali Katika Maeneo ya Vijijini

### Ardhi Itupatie Mahitaji Yetu

Kwa mibaraka yake Mungu, ardhi hii ikilimwa itatupatia mahitaji yetu. Tusikate tamaa kwa mambo ya maisha haya kwa sababu ya kuonekana hali ile ya kushindwa, wala tusivunjike moyo kwa kuchelewa mambo. Yatupasa kuulima udongo kwa furaha, matumaini, na shukrani, tukisadiki ya kwamba ndani ya udongo huo kuna hazina nyingi za kuweka ghalani mwetu kwa mfanyakazi mwaminifu, yaani, hazina zile zenye utajiri mwingi kuliko dhahabu na fedha. Shutuma ile inayotolewa kwake [huo udongo] kuwa ni mnyimivu [hautupatii mavuno ya kutosha] ni ya uongo. Kwa kuilima vizuri na kutumia akili ardhi itatoa hazina zake [mazao] kwa manufaa ya mwanadamu. Milima na vilima hubadilika; dunia huchakaa kama vazi kuukuu; lakini mbaraka wa Mungu, unaoandaa meza [chakula] jangwani kwa ajili ya watu wake, hautakoma kamwe.

Nyakati ngumu sana zi mbele yetu, tena ipo haja kubwa kwa familia kutoka mijini kwenda kule shamba [vijijini], kweli yaweza kupelekwa katika vichochoro sawasawa tu na vile inavyoweza kupelekwa katika njia kuu za usafiri za dunia hii. Mengi hutegemea juu ya kupanga mipango yetu kulingana na Neno la Bwana, na kwa juhudi ya kudumu kuitekeleza [mipango hiyo]. Mambo mengi sana hutegemea bidii yetu iliyotolewa wakf pamoja na ustahimilivu wetu kuliko kutegemea akili nyingi isiyo ya kawaida na maarifa yale yapatikanayo katika vitabu ambayo hayatendewi kazi. Talanta zote na uwezo wote aliowapa mawakala wake wa kibinadamu, visipotumika, basi, havina faida yo yote kwetu.

Kuzirudia njia zile rahisi [za utendaji kazi] kutathaminiwa na watoto na vijana wetu. Kazi ya bustanini na shambani italeta badiliko linalokubalika badala ya kawaida zile zinazochosha sana za masomo ya kinadharia, ambayo akili za watoto wao wadogo zisingejihusisha nayo kwa muda mrefu. Kwa mtoto mdogo aliye dhaifu kiakili, ambaye anaona masomo ya vitabuni kuwa yanamchosha sana, na kwake huwa ni vigumu kuyakumbuka, kazi kama hiyo itakuwa na manufaa ya pekee kwake. Kuna afya na furaha kwa ajili yake katika kujifunza maumbile [viumbe vya asili]; na picha inayozama moyoni mwake haitaweza kufifia, kwa maana mambo hayo yatahusishwa na vitu vile vilivyo mbele ya macho yake daima. ----- Testimonies, Gombo la 6, uk. 178,179. (1900)

### Mkiwa na Kipande Kidogo cha Ardhi na Nyumba Nzuri ya Kuishi

Ardhi inapaswa kushughulikiwa mpaka iweze kutoa nguvu yake; lakini pasipo kuwapo mbaraka wa Mungu haiwezi kutoa kitu. Hapo mwanzo, Mungu aliangalia vyote alivyoviumba, na kusema

kwamba vilikuwa vyema sana. Laana ililetwa juu ya nchi [udongo] kama matokeo ya dhambi. Lakini, je! laana hiyo izidi kuongezeka kwa kuzidi kufanya dhambi? Ujinga unaendelea kuleta matokeo yake yanayoleta madhara mengi. Watumishi walegevu [wavivu] wanazidisha maovu kwa tabia zao za kivivu. Wengi hawako tayari kujipatia chakula chao kwa jasho la uso wao, wanakataa kuilima ardhi. Lakini ardhi inazo hazina zake zilizojificha chini kwa ajili ya wale walio na ujasiri na nia na uvumilivu wa kuzikusanya hazina zake hizo. Akina baba na mama walio na kipande cha ardhi na nyumba nzuri ya kuishi, hao ni wafalme na malkia.

Wakulima wengi wameshindwa kupata mavuno ya kutosha kutoka katika mashamba yao kwa sababu wameichukulia kazi hiyo kana kwamba ni kazi ya kudhalilisha mno; hawatambui kwamba kuna mbaraka ndani yake kwa ajili yao wenyewe na familia zao. Yale yote wanayofahamu wao ni kwamba kazi hiyo ni utumwa wa aina fulani. Mashamba yao ya miti izaayo matunda huachwa bila kutunzwa, mazao hayapandwi kwa majira yake yanayofaa, na kazi ya juu juu tu hufanywa katika kuilima ardhi hiyo. ----- Fundamentals of Christian Education, uk. 326,327. (1894)

## Matunda, Mboga za Majani, na Kuku Vyapendekezwa kwa Eneo Moja

Katika ujirani huu kuna eneo kubwa la ardhi isiyokaliwa na watu. Baadhi ya watu wetu wanaoishi katika mazingira ya hali ya hewa iliyosumishwa huko mijini wangeweza kunufaika kwa kujipatia ekari chache za ardhi hii. Wangeweza kujipatia mahitaji yao ya maisha kwa kupanda matunda na mboga za majani na kufuga kuku. Hospitali yetu ingefurahi kununua mayai na mboga za majani kutoka kwao. Natamani kwamba mradi fulani kama huo ungeanzishwa hapa. Baraka kubwa ingewajia wazazi hao pamoja na watoto wao, endapo wangeondoka katika miji hiyo miovu, iliyochafuliwa na kwenda katika sehemu zile za shamba [vijijini]. ----- Letter 63, 1904.

## Kuishi Mashambani [Vijijini] - Mbaraka Kwa Maskini

Endapo maskini ambao hivi sasa wamesongamana mijini wangepata makazi yao huko mashambani [vijijini], wasingeweza kujipatia riziki yao tu, bali wangepata afya na furaha ambayo mpaka sasa hawaijui. Mara nyingi [huko mijini] kazi ngumu, chakula duni, na kubana mno matumizi, shida na umaskini, hiyo ndiyo ingekuwa sehemu ya maisha yao. Lakini ni mbaraka ulioje ambao ungekuwa wao kama wangeondoka mjini, na kuviachilia mbali vishawishi vyake vinavyowaelekeza watu maovuni, kuachana na machafuko yake na uhalifu, huzuni na uchafu wake, na kwenda mashambani [vijijini] kwenye utulivu na amani na usafi.

Kwa wengi miongoni mwa wale wanaoishi mijini ambao hawana hata kipande kidogo cha majani mabichi cha kuweza kuweka miguu yao juu yake, ambao mwaka nenda mwaka rudi wameziangalia nyua zao zilizojaa uchafu na njia zile finyu za vichochoroni, kuta zile za matofali ya kuchoma na

sakafu za mawe za kutembea juu yake, mbingu zile zilizojaa vumbi na moshi, ----- kama hao wangepelekwa kwenye wilaya moja yenye mashamba ya kulima, yaliyozungukwa na mashamba ya chanikiwiti, misitu midogo, na vilima na vijito, mbingu safi na zenye hewa safi, na hewa safi ile ya mashambani, basi, kwao hao ingekuwa karibu sawa na [kuishi] mbinguni.

Mawasiliano yao yakiwa yamekatwa kwa kiwango kikubwa hata wasiweze kuonana na watu wengine wala kuwategemea, tena wakiwa wametengwa mbali na semi zile chafu za ulimwengu pamoja na desturi zake na misisimko yake, wangeweza kukaribia sana kwenye maana ya ndani kabisa ya maumbile. Kuwako kwake Mungu kungesikika na kuwa dhahiri sana kwao. Wengi wangejifunza kwake fundisho lile la kumtegemea yeye. Kupitia katika maumbile hayo wangeweza kuisikia sauti yake mioyoni mwao ikiwatamkia amani na upendo wake, na akili na roho na mwili wao vingeweza kuitikia uponyaji huo, ulio na uwezo wa kuwapa uzima. ----- The Ministry of Healing, uk. 190-192. (1905).

## Viwanda Vidogo Mbalimbali Kwa Familia Zitokazo Mijini

Waumini wale ambao kwa sasa wanaishi mijini inawapasa kwenda shamba [vijijini], ili wapate kuwaokoa watoto wao na maangamizi. Mawazo yanapaswa kuelekezwa upande wa kuanzisha viwanda [vidogo] ambamo familia hizo zinaweza kupata kazi. Wale wanaosimamia kazi ya Shule na wangeona kile kinachoweza kufanywa na taasisi hizo zingeweza kuanzisha viwanda [vidogo] kama hivyo, ili watu wetu wanaotaka kuondoka mijini, waweze kujipatia makazi yao yanayofaa bila kutumia fedha nyingi sana, na pia kuweza kupata kazi huko. Katika sehemu zote mbili na kuna hali nzuri ya ardhi ambayo inatia moyo kuweza kuuendeleza mpango kama huo. Jifunzeni hali ya nchi ilivyo.

Yale yote yanayotakiwa kufanywa hayawezi kuelezwa kinagaubaga mpaka hapo mwanzo utakapofanywa. Liombeeni jambo hilo, tena kumbukeni kwamba Mungu ameshika usukani, kwamba yeye ndiye anayeongoza katika shughuli zote za kibiashara. Mahali pale kazi inapoendeshwa kwa njia inayotakiwa panakuwa fundisho la mfano linalopaswa kuigwa na mahali pengine [patakapofunguliwa]. Pasiwe na ufinyu wo wote [wa mawazo], wala ubinafsi, katika kazi hiyo inayofanyika mahali hapo. Kazi hiyo inatakiwa kuwekwa juu ya msingi rahisi, unaoweza kutekelezwa. Wote hawana budi kufundishwa ya kuwa sio tu kukiri kwamba wanaiamini kweli, kama vile kweli yenyewe ilivyo, bali kuionyesha kweli hiyo kwa mfano katika maisha yao ya kila siku. ----- Letter 25, 1902.

## Kazi ya Kuuza Chakula Kiletacho Afya

Shughuli [biashara] hiyo ya [kuuza] chakula kiletacho afya inapaswa kuanzishwa hapa [Avondale]. Hiyo ingekuwa mojawapo ya viwanda vinavyohusiana na Shule. Mungu ameniagiza mimi kwamba wazazi wanaweza kupata kazi katika kiwanda hicho, na kuwapeleka watoto wao shuleni. Lakini kila kitu kinachofanyika hapo kinapaswa kufanywa kwa njia iliyo rahisi sana. Pasiwepo na ubadhirifu [matumizi mabaya] wo wote katika jambo lo lote lile. Kazi thabiti inapaswa kufanywa, kwa sababu kazi isipofanywa kwa uthabiti, matokeo yake yatakuwa kazi ya ovyo ovyo tu. ----- Australasian Union Conference Record, Julai 28, 1899.

# SEHEMU YA TANO

## Kujiandaa kwa Hatari Kubwa Itakayoletwa na Amri ya Jumapili

### Nyakati za Taabu Ziko Mbele Yetu

Haitupasi sisi kujiweka wenyewe mahali ambapo tutalazimishwa kuwa na uhusiano wa karibu sana na wale wasiomheshimu Mungu.... Hatari kubwa karibu sana inakuja kuhusiana na utunzaji wa Jumapili....

Kundi la Jumapili linajiimarisha lenyewe katika madai yake ya uongo, na jambo hilo litamaanisha mateso kwa wale wanaokata shauri kuitunza Sabato ya Bwana [Jumamosi]. Yatupasa kujiweka wenyewe mahali pale tutakapoweza kuishika amri hiyo ya Sabato [Jumamosi] kwa ukamilifu wake. "Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote." Tena yatupasa kuwa waangalifu tusijiweke mahali pale itakapokuwa vigumu kwetu sisi wenyewe na watoto wetu kuitunza Sabato [Jumamosi].

Endapo kwa maongozi yake Mungu tunaweza kujipatia mahali pa kuishi mbali na miji, basi, Bwana angependa kwamba sisi tufanye hivyo. Nyakati za taabu ziko mbele yetu. ----- Manuscript 99, 1908.

## Harakisheni Kujiweka Tayari

Uwezo waliopewa wafalme [Ma-Rais] ukifungamana na wema ni kwa sababu yule aliyeshika madaraka hayo yuko chini ya uongozi wa Mungu. Uwezo huo unapofungamana na uovu, basi, unafungamana na nguvu za Shetani, nao utafanya kazi ya kuwaangamiza wale walio mali yake Bwana. Ulimwengu wa Kiprotestanti umeisimamisha sanamu ya sabato [Jumapili] mahali pale ambapo Sabato ya Mungu [Jumamosi] ingepaswa kusimama, nao wanatembea katika nyayo za Upapa. Kwa sababu hiyo mimi nauona umuhimu kwa watu wa Mungu kuondoka mijini kwenda kwenye sehemu za upweke huko mashambani [vijijini], ambako wanaweza kulima mashamba yao na kuzalisha wenyewe mazao yao. Kwa njia hiyo wanaweza kuwalea watoto wao kuwa na tabia ya kawaida, inayoleta afya. Nauona umuhimu wa kuharakisha kuyaweka mambo yote tayari ili kuweza kukabiliana na hatari hiyo kubwa. ----- Letter 90, 1897.

## SURA YA SITA

## Tusikae Wengi Mahali Pamoja Katika Vituo Vya Taasisi Zetu

### Tusikae Wengi Mahali Pamoja

Katika siku zetu hizi Bwana anataka watu wake watawanyike ulimwenguni kote. Haiwapasi kukaa wengi mahali pamoja. Yesu alisema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe [mtu]." Marko 16:15. Wanafunzi walipofuata mapenzi [matakwa] yao ya kubaki kwa idadi kubwa kule Yerusalemu, mateso yaliruhusiwa kuwapata, nao wakatawanyika kwenda mahali pote katika ulimwengu ule uliokaliwa na watu.

Kwa miaka mingi ujumbe huu wa onyo na wa kuwasihi umekuwa ukija kwa watu wetu, ukiwashurutisha kusonga mbele na kuingia katika shamba la Bwana la mavuno, na kufanya kazi bila kujifikiria wenyewe kwa ajili ya roho za watu. ----- Testimonies, Gombo la 8, uk 215. (1904)

### Tawanyikeni Na Kwenda Kule Wasikolipata Onyo Hilo

Washiriki wa makanisa yetu makubwa ni wengi ambao karibu hawafanyi kitu cho chote kabisa. Hao wangeweza kufanikiwa kufanya kazi nzuri kama wangeweza kutawanyika na kwenda mahali ambako kweli hii bado haijaingia badala ya kujikusanya wengi mahali pamoja. Miti iliyopandwa karibu karibu sana haisitawi. Hupandikizwa mahali pengine na mwenye bustani ili ipate nafasi ya kutosha kukua, isizuiwe kukua zaidi wala isiwe dhaifu. Kanuni iyo hiyo ingefanya kazi yake vizuri kwa makanisa yetu makubwa. Wengi miongoni mwa washiriki wetu wanakufa kiroho kwa kukosa kazi hii hii [ya kwenda mahali kule ambako ujumbe bado haujafika]. Wanakuwa dhaifu, tena

wanashindwa kufanya kazi yao vizuri. Wangepandikizwa [wangehamia] mahali pengine, wangeweza kupata nafasi ya kutosha kuweza kukua [kiroho] na kuwa na nguvu.

Si kusudi lake Mungu kwamba watu wake wakae wengi mahali pamoja, au waishi pamoja katika jumuia kubwa. Wanafunzi wa Yesu ni wawakilishi wake hapa duniani, na Mungu anakusudia kwamba wao watatawanyika kila mahali duniani, katika miji midogo, miji mikubwa, na vijijini, na kuwa kama mianga kati ya giza nene la ulimwengu huu. Wanapaswa kuwa wamishonari wa Mungu, kwa imani yao wakishuhudia ukaribu sana wa marejeo ya Mwokozi wao.

## MAHALI PALE ILIPOFUNGUKA NJIA YA KUJIPATIA RIZIKI

Washiriki walei [wa kawaida] wa makanisa yetu wanaweza kufanikiwa kufanya kazi ile ambayo, hata sasa, hawajaanza kuifanya. Wasiwepo watu wanaohamia mahali papya kwa ajili ya faida ya kidunia tu; bali mahali pale ilipofunguka njia ya kujipatia riziki ziende familia zile zilizojizatiti katika kweli, familia moja au mbili hivi ziende mahali pamoja kufanya kazi kama wamishonari. Wangejisikia kuwa wanayo haja ya kuwapenda watu, kwamba wanao mzigo wa kuwashughulikia watu hao, tena, kama somo lao, wangejifunza namna ya kuwaingiza katika kweli hii. Wanaweza kugawa vitabu vyetu, kufanya mikutano nyumbani mwao, kufahamiana na majirani zao, na kuwaalika waje kwenye mikutano hiyo. Wanaweza kuiacha nuru yao kuangaza kwa matendo yao mema. ----- Testimonies, Gombo la 8, uk. 244,245. (1904)

## Vishawishi Vya Taasisi Zetu Visiwavute

Wale wanaojisikia kupenda kuishi karibu na nyumba yetu ya kuchapisha vitabu au hospitali na shule yetu iliyo kwenye bustani ile kubwa ya Takoma [Takoma Park] hawana budi kupata ushauri kabla hawajahamia huko.

Kwa wale wanaotarajia kwenda kule Mountain View kama ndipo mahali pazuri pa kuishi, ati kwa sababu tu mtambo wetu wa kuchapisha vitabu wa Pasifiki [Pacific Press] utajengwa pale, ningependa kuwaasa hivi: Zitupieni macho sehemu nyingine za ulimwengu zinazohitaji nuru yenu mliyoipokea kama amana. Kumbukeni kwamba Mungu amempa kila mtu kazi yake. Chagueni mahali fulani mtakapokuwa na nafasi nzuri ya kuiacha nuru yenu kuangaza kati ya giza hilo la kimaadili.

Inatokea sikuzote ya kwamba taasisi yetu inapojengwa mahali fulani, ziko familia nyingi zinazotaka kwenda huko na kuweka makao yao karibu nayo. Hivyo ndivyo ilivyokwisha kutokea kule Battle Creek na Oakland, na, kwa kiwango fulani, karibu kila mahali ambapo tunayo shule au hospitali yetu. ----- Fundamentals of Christian Education, uk. 494,495. (1904).

## Msianzishe Vituo Vya Yerusalemu

Watu wetu ... hawapaswi kupaangalia ... kama kituo cha Yerusalemu. Wasifikiri kwamba kwa sababu idadi fulani ya ndugu zetu wameitwa kuja hapa kujiunga na kazi hii ya uchapishaji, basi, hapa ndipo mahali pa kukaa idadi kubwa ya watu wetu na familia zao. Na kila mtu anayehusika na Ofisi hiyo ajiweke tayari kuondoka endapo Mungu atamwita kwenda mahali fulani papya. ----- Manuscript 148, 1905.

Msisongamane mahali pamoja, mkifanya kosa lile lile lililokwisha kufanywa kule Battle Creek. Kuna mamia ya mahali pengine panapohitaji nuru hiyo aliyowapa Mungu. ----- Fundamentals of Christian Education, uk. 495. (1904).

## Bakini Katika Makanisa Madogo - Anzisheni Shule Nyingi Mpya

Familia nyingi ambazo, kwa madhumuni ya kuwapatia elimu watoto wao, huhamia mahali kule zilikojengwa shule zetu kubwa, wangeweza kufanya kazi bora kwa ajili ya Bwana kwa kuendelea kubaki pale pale walipo. Wangelitia moyo kanisa ambalo wao ndio washiriki wake kujenga shule ya kanisa ambayo watoto walio katika mipaka yake wangeweza kujipatia elimu kamili ya Kikristo itakayowawezesha kufanya kazi yao. Lingekuwa ni jambo bora sana kwa watoto wao, kwao wenyewe, na kwa kazi ya Mungu, kama wangeendelea kubaki katika makanisa hayo madogo, ambamo msaada wao unahitajika badala ya kwenda kule yaliko makanisa yetu makubwa, ambako, kwa vile wao hawahitajiki [hawatakuwa na kazi kanisani], kuna majaribu daima ya kuanguka katika uzembe [uvivu] wa kiroho.

Po pote pale walipo Wasabato wachache, wazazi wangeungana pamoja na kutenga eneo kwa ajili ya shule ya kutwa ambamo watoto na vijana wao wanaweza kupata mafunzo yao. Wamwajiri mwalimu Mkristo, ambaye, kama mmishonari aliyejitoa wakf, ataweza kuwaelimisha watoto wao kwa njia ambayo itawafanya nao wawe wamishionari. ----- Counsels to Teachers, uk. 173,174. (1913)

## Hivi Malaika Wanajisikiaje

Nafikiria jinsi malaika wanavyojisikia wanapouona mwisho ule ukikaribia, na kuwaona wale wanaodai kuwa wanayo maarifa ya kumjua Mungu na Yesu Kristo aliyemtuma, wakisongamana sana mahali pamoja, wakikaa wengi mahali pamoja, na kuhudhuria mikutano yao, na kuwa na hisia ya kukata tamaa na kutoridhika endapo hakuna mahubiri mengi yanayozinufaisha roho zao na kuliimarisha kanisa, wakati wao hawafanyi kazi yo yote kabisa. ----- Letter 16e, 1892.

Ipanueni Kazi na Kuieneza - Ila Sio Pale Makao Makuu

Watu wanahamasishwa [wanatiwa moyo] kulundikana pale Battle Creek, tena wanalipa zaka yao na kutoa mvuto wao ili ipate kujengwa Yerusalemu ya leo pale ambayo haifuati mpango wa Mungu. Kwa kufanya kazi hiyo mahali pengine panakosa msaada ambao wangeweza kuupata. Panueni kazi, enezeni, naam; lakini sio mahali pamoja. Tokeni na kujenga vituo vyenye mvuto mahali pale ambapo hakuna kitu au karibu hakuna cho chote kilichofanyika pale. Livunje-vunjeni kundi hilo kubwa sana lililosongamana mahali pamoja; tawanyeni miali ya nuru ile iokoayo, na kuiangaza nuru hiyo katika pembe [kona] za dunia zilizotiwa giza. ----- Testimonies to Ministers, Uk. 254,255. (1895)

## SEHEMU YA SABA

## Kuongozwa na Maongozi ya Mungu

### Mungu Anapoifungua Njia

Wakati umefika, ambapo, kadiri Mungu anavyoifungua njia, familia hazina budi kutoka mijini. Watoto wapelekwe kule shamba [vijijini]. Wazazi na wajipatie mahali panapofaa kulingana na fedha walizo nazo zitakavyoruhusu. Ingawa nyumba ile iliyojengwa inaweza kuwa ndogo, hata hivyo, pangekuwapo na shamba linaloweza kulimwa kuambatana nayo. ----- Manuscript 50, 1903.

### Mungu Atawasaidia Watu Wake

Wazazi wanaweza kujijengea nyumba ndogo huko shamba [vijijini], na kuwa na mashamba ya kulima, ambamo wanaweza kuwa na viunga vya miti ya matunda, na kupanda mboga za majani pamoja na matunda madogodogo ili kuchukua mahali pa nyama, ambayo inaichafua sana damu inayopita katika mishipa na kuleta uzima. Mahali hapo watoto hawatazungukwa na mivuto ile

miovu ipatikanayo katika maisha yale ya mjini. Mungu atawasaidia watu wake kupata makazi kama hayo nje ya miji [wakimwomba]. ----- Medical Ministry, uk. 310. (1902)

## Kusaidia Kuifungua Njia

Wakati unapozidi kusonga mbele, watu wetu wengi zaidi na zaidi watalazimika kuihama miji. Kwa miaka mingi tumeagizwa ya kwamba ndugu na dada zetu, na hasa familia zile zenye watoto, wangefanya mpango wa kuondoka mijini kwa kadiri njia inavyofunguka mbele yao na kuwawezesha kufanya hivyo. Wengi watalazimika kufanya kazi ngumu kwa bidii ili kusaidia kuifungua njia. Lakini mpaka hapo itakapowezekana kwao kuhama, kadiri wanavyoendelea kubaki humo, wangefanya bidii kubwa sana kufanya kazi ya umishonari, haidhuru eneo la mvuto wao liwe dogo jinsi gani. ----- Review and Herald, Sept. 27, 1906.

## Ushauri na Onyo Kwa Wale Wanaotarajia Kuondoka Mijini

[Barua hii iliandikwa Desemba 22, 1893, kuijibu barua iliyotoka kwa kiongozi maarufu wa Battle Creek, akimjulisha Bibi White kuwa kama itikio lao kwa onyo lile linalowataka watu wetu kuhama kutoka Battle Creek, "kati ya watu mia moja na mia mbili" hivi walikuwa wanajiandaa kuondoka "kwa haraka iwezekanavyo." ----- WAKUSANYAJI WA MAANDIKO.]

Ndugu yangu, barua yako inaniambia kwamba wapo wengi waliopata mwamko mkubwa wa kuondoka Battle Creek. Ipo haja, haja kubwa, ya kazi hiyo kufanyika, na kufanyika sasa. Wale wanaojisikia kuhama hivi mwishoni hebu isiwe kwa kukurupuka, kwa msisimko, au bila kufikiri, au kwa njia ambayo hatimaye watajuta sana kuhama kwao....

Angalieni sana pasiwepo na kuhama kunakofanywa bila kufikiri katika kulitii onyo hilo la kuhama kutoka Battle Creek. Msifanye jambo lo lote bila kuitafuta hekima toka kwa Mungu, ambaye ameahidi kuwapa kwa ukarimu wale wote wamwombao, na ambaye hakemei [Yakobo 1:5]. Yale yote ambayo mtu ye yote anaweza kufanya ni kuwapasha habari tu na kutoa ushauri wake, kisha kuwaacha wale wanaoamini kwa dhati kuhusu wajibu wao wa kuhama, wakiwa chini ya uongozi wake Mungu, kufanya hivyo; mioyo yao yote ikiwa imefunguliwa wazi ili wapate kujifunza na kumtii Mungu.

Mimi nasumbuka sana moyoni mwangu kufikiri kwamba huenda wapo hata baadhi ya waalimu [wachungaji, n.k.] wetu ambao wanahitaji kuwa na busara zaidi ili waweze kufikiria pande zote [za jambo hilo]. Wajumbe wale wanaouchukua ujumbe huo wa rehema kwa ulimwengu wetu, ambao wanategemewa na watu wetu, wataombwa kutoa mawaidha [maoni] yao. Tahadhari kubwa haina budi kutumika kwa upande wa watu hao ambao hawana uzoefu halisi wa maisha ya kujitegemea

[vijijini] kwa kufanya kazi [kwa mikono yao], na ambao watakuwa hatarini kutoa mawaidha yao, wasijue mawaidha yao hayo yatasababisha watu wengine kufanya kitu gani.

## KIPAWA CHA KUTOA USHAURI

Watu wengine wanaona mbali katika mambo mengi, hao wanao uwezo wa kutoa ushauri. Ni kipawa cha Mungu. Katika nyakati zile ambazo kazi ya Mungu inahitaji maneno ya busara na ya dhati, na yale yaliyo thabiti, hao wanaweza kusema maneno fulani ambayo yatawafanya watu wale waliochanganyikiwa pamoja na wale walio gizani [wasioelewa kitu], kuiona kwa ghafula, kama vile nuru ya mwanga wa jua inavyomulika ghafula, njia ile wanayopaswa kuifuata katika jambo lile lililowajaza mashaka mengi na kuifadhaisha sana mioyo yao wakati walipokuwa wakifanya uchunguzi wao uliowachukua majuma mengi na miezi mingi. Ufumbuzi upo, yaani, ufyekaji wa njia ile iliyo mbele yao, na Mungu ameruhusu mwanga wake wa jua kuingia mawazoni mwao, nao wanaona ya kuwa maombi yao yamejibiwa, yaani, njia yao iko wazi. Lakini basi, mawaidha fulani yanaweza kutolewa bila kufikiri, yakisema ----- tokeni tu Battle Creek, wakati hakuna maelezo yo yote yaliyofafanuliwa vizuri kuhusu maendeleo gani watakayofanya katika maisha yao ya kiroho kwa ajili yao wenyewe au kwa ajili ya wengine kwa kuichukua hatua hiyo [ya kuhama].

## FIKIRIENI KWA MAKINI SANA KILA HATUA YA KUHAMA KWENU

Hebu kila mmoja awe na muda wa kutosha wa kufikiria [jambo hilo] kwa makini [uangalifu] sana; asije akafanana na mtu yule aliyetajwa katika mfano [wa Yesu] aliyeanza kujenga, kisha akashindwa kumaliza. Kuhama ko kote kusifanyike isipokuwa kama kuhama huko na matokeo yake yote yamefikiriwa kwa makini sana ----- yaani, kila jambo limepimwa kuona uzito wake... Kwa kila mtu kazi ilitolewa kulingana na uwezo wake. Basi, asihame akiwa na mashaka, bali ajizatiti, na wakati uo huo akiwa ananyenyekea kwa kumtegemea Mungu.

Huenda wakawapo watu ambao watataka kuharakisha kufanya jambo fulani, na kujiingiza katika shughuli fulani ambayo hawaijui kabisa. Mambo hayo Mungu hataki. Fikiri kwa moyo mnyofu, kwa maombi, ukijifunza Neno [la Mungu] kwa makini sana na kwa maombi, akili yako na moyo wako vikiwa tayari kuisikiliza sauti ya Mungu.... Kuyajua mapenzi ya Mungu [katika suala hili] ni jambo kubwa.

## MIPANGO ILIYOPANGWA VIZURI INATAKIWA

Nayatoa maneno haya kwa kanisa lile lililoko kule Battle Creek ili lipate kutembea katika mashauri ya Mungu. Haja ipo ya kuhama kwenu ----- yaani, wengi wenu kuhama kutoka Battle Creek ----- tena, ipo haja pia ya ninyi kuwa na mipango iliyopangwa vizuri juu ya kile mtakachofanya mtakapohama toka Battle Creek. Msiende kwa kukimbia, bila kujua mnachofanya.... Laiti kama wangekuwapo majenerali wenye hekima, wanaowafikiria wengine, watu wale wanaoyachunguza mambo kwa kuangalia kila upande, watakaokuwa washauri salama, ambao kidogo wanajua kile kilichomo ndani ya mwanadamu, wale ambao wanajua kuongoza na kushauri katika kicho chake Bwana.

## HATARI INAAMBATANA NA UZOEFU MPYA

Nimekwisha kuona kwamba hatari inaambatana na kila awamu mpya ya uzoefu kanisani, kwa sababu wengine wanayasikia mambo hayo kwa moyo wenye kusisimka sana. Wakati waalimu [wachungaji, n.k.] wengine wanaweza kuwa imara upande ule wa kufundisha mafundisho ya Biblia, si wote watakaokuwa wamepata uzoefu wa maisha ya kujitegemea, si wote watakaowashauri wale waliochanganyikiwa kwa hakika na usalama. Hawaitambui hali hiyo ya kutatanisha ambayo haina budi kuja kwa kila familia itakayofanya mabadiliko hayo. Kwa hiyo, wote wawe waangalifu sana kuchunga maneno yao wanayosema; kama hawayajui mawazo ya Mungu katika baadhi ya mambo, basi, wasiseme kabisa kwa kukisia-kisia tu au kwa kudhani kuwa mambo hayo yako hivyo. Kama hawajui kitu cho chote kilicho dhahiri, hebu na waseme hivyo, na kuwaacha watu kila mmoja peke yake wapate kumtegemea Mungu. Hebu maombi mengi yafanyike, hata kwa kufunga, ili mtu ye yote asije akahama akiwa gizani [hajui la kufanya], bali ahame akiwa nuruni [anajua la kufanya] kama vile Mungu alivyo nuruni....

## HAMENI KWA HADHARI

Hebu pasiwepo na kitu cho chote kinachofanywa bila utaratibu, isije ikatokea hasara kubwa au kupoteza mali kwa sababu ya hotuba motomoto zilizotolewa zenye kujaa misisimko ndani yake ambazo zinaamsha shauku ambayo haimo katika mpangilio wa Mungu, hata ushindi ule uliokuwa wa lazima kupatikana uweze kugeuka na kuwa kushindwa kunakotokana na kukosa utulivu wa kusimamia mambo vizuri na kuyafikiria vizuri, na kujenga juu ya kanuni na makusudi yaliyo imara. Hebu na pawepo na uongozi wa busara katika jambo hilo, na wote wapate kuhama chini ya uongozi ule wenye hekima wa Mshauri yule asiyeonekana, ambaye ni Mungu. Mambo ya kibinadamu yatajitahidi kutawala, na huenda pakawa na kazi iliyofanyika ambayo haina sahihi [idhini] ya Mungu. Basi, namsihi kila mtu asiwaangalie washiriki hao wa kibinadamu kwa nia na

imani thabiti sana, bali amwangalie kwa bidii nyingi sana Mungu, mshauri mmoja aliye a hekima. Wekeni njia zenu zote na mapenzi [nia] yenu ili yapatane na njia za Mungu na mapenzi yake....

## MATOKEO YA HATUA ZA HARARA

Endapo wengine watahama kwa haraka na kukimbia toka Battle Creek, halafu wakajikuta wameingia katika hali ya kukata tamaa, basi, watatoa shutuma zao, sio juu yao wenyewe, kwa kuhama kwao bila kutumia busara, bali juu wa wengine, ambao watawalaumu kuwa walitia shinikizo lao juu yao [mpaka wakawa wamehama]. Kutibuliwa kwa mipango yao yote na kushindwa kwao kutawafanya wawarudishie shutuma zote wale ambao wasingestahili kupewa sifa mbaya kama hizo....

Sasa, hivi sasa, ndio wakati ambao hatari zile kubwa za siku za mwisho zinazidi kuongezeka sana kutuzunguka pande zote, tunahitaji watu wenye hekima kuwa washauri wetu, sio watu wale watakaoona kwamba ni wajibu wao kuwasisimua watu na kuleta machafuko, bali ni wale wawezao kutoa mashauri yao ya busara na kuratibu na kupanga mipango ili kwamba kila msisimko unaotokea upate kuleta mpangilio mzuri kutoka katika machafuko yaliyopo, na kuleta raha na amani kwa njia ya kulitii Neno la Bwana. Hebu kila mtu na apatikane mahali pake panapomfaa hasa, ili apate kumfanyia Mungu kazi fulani, kulingana na uwezo wake aliopewa....

Kwa jinsi gani jambo hilo litaweza kufanyika? "Jitieni nira yangu," asema Yesu Kristo, yule aliyewanunua ninyi kwa damu yake ya thamani, ninyi ambao ni watumishi na mali yake, "mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." Endapo kila mmoja atakuja kwa Yesu akiwa na moyo ulio tayari kufundishwa, moyo wenye toba, hapo ndipo atakuwa katika hali ya kiakili ya kuweza kufundishwa na kujifunza kwa Yesu na kuyatii maagizo yake....

## WEKENI KILA MPANGO MLIO NAO MBELE ZAKE MUNGU

Hatuwezi kuwa na imani dhaifu sasa; hatuwezi kuwa salama kwa kuwa na mtazamo ulio mlegevu, wa kivivu, na wa kizembe. Kila chembe ya nguvu yetu inapaswa kutumika, na fikira kali, tulivu, zenye kina zinapaswa kutumika. Hekima ya mjumbe ye yote wa kibinadamu haitoshi katika kupanga mipango na kubuni mbinu kwa wakati kama huu. Wekeni kila mpango mlio nao mbele zake Mungu kwa kufunga pamoja na kujinyenyekeza nafsi zenu mbele zake Bwana Yesu, na kuzikabidhi njia zenu kwa Bwana. Ahadi ya hakika ni hii, "Naye atayanyosha mapito yako [Atakuongoza katika njia zako - Mithali 3:5,6]. Yeye hana kikomo katika uwezo wake wa kusaidia. Mtakatifu wa Israeli, anayeliita jeshi lote la mbinguni kwa majina yake, na kuzishikilia nyota za mbinguni mahali pake, anawatunza ninyi kila mmoja peke yake....

Ningependa kwamba wote wapate kutambua uwezekano na mwelekeo uliopo kwa wale wote wanaomfanya Kristo kuwa utoshelevu wao na tegemeo lao. Uhai ule uliofichwa pamoja na Kristo katika Mungu daima unalo kimbilio; mtu huyo anaweza kusema, "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."

Jambo hili nawaachieni mikononi mwenu; kwa maana nimekuwa na wasiwasi na kusumbuka sana kwa ajili ya hatari zile zinazowashambulia wote walioko huko Battle Creek, ili wasije wakahama bila kuwa na tahadhari kubwa na [kwa kufanya hivyo] kumpa yule adui yetu faida kubwa. Jambo hilo halipaswi kuwa hivyo, maana kama tukienda kwa unyenyekevu na Mungu wetu, basi, tutakwenda salama. ----- Letter 45, 1893.

# SURA YA NANE

## Vituo Vyetu vya Taasisi Kuwa Mbali na Msongamano wa Watu

### Mahali Panapofaa Kujenga Taasisi Zetu

Agizo [lile lile] bado linazidi kutolewa, Tokeni mijini. Jengeni hospitali zenu, shule zenu, na ofisi zenu mbali na vituo vyenye watu wengi. Wengi kwa wakati huu wanaomba sana ili wapate kubakia mijini, lakini wakati utakuja, muda si mrefu kuanzia sasa, ambapo wale wote wanaotaka kuziepuka tamasha na sauti hizo za uovu watakapohama na kwenda shamba [vijijini]; kwa maana uovu na uchafu utaongezeka kwa kiwango ambacho mazingira yote ya mjini yataonekana kana kwamba yamechafuliwa. ----- Letter 26, 1907.

### Kuepuka Majaribu na Ufisadi

Wengine wameshangaa kwa nini ofisi yetu ya uchapishaji inatakiwa kuhamishwa toka Oakland kwenda Mountain View. Mungu amekuwa akiendelea kuwaita watu wake kuondoka mijini. Vijana wetu ambao wamefungamana na taasisi zetu hawapaswi kuwekwa mahali pale watakapoweza kukabiliwa na majaribu na ufisadi unaoonekana katika miji mikubwa. Mountain View pameonekana kuwa ni mahali panapofaa kwa ofisi yetu ya uchapishaji. ----- Manuscript 148, 1905.

## Nyakati za Dhoruba Zi Mbele Yetu

Janga hilo [la kuteketezwa kwa moto jengo la Review and Herald] linaweza kuleta mabadiliko dhahiri katika mambo yetu. Natumaini kwamba ndugu zetu hao watalizingatia fundisho hilo ambalo Mungu anataka kuwafundisha, na ya kwamba hawatarudia kuijenga tena nyumba ya uchapishaji pale Battle Creek. Mungu anamaanisha kwamba sisi hatutakaa mijini; maana zinakuja nyakati za dhoruba kali sana mbele yetu. ----- Letter 2, 1903.

## Mahali Wanapoweza Kufundishwa Kwa Ufanisi Vijana Wetu

Mungu ametuma kwetu onyo baada ya onyo ya kwamba shule zetu na nyumba zetu za uchapishaji pamoja na hospitali zetu hazina budi kujengwa nje ya mji, mahali wanapoweza kufundishwa kwa ufanisi vijana wetu kuhusu kweli ni nini. Asiwepo mtu ye yote anayezitumia Shuhuda [zangu] kutetea ujenzi wa shughuli zetu kubwa za kibiashara mijini. Msiitangue nuru iliyokwisha kutolewa kwetu juu ya somo hilo.

Watu watainuka [watatokea] wakisema mapotovu, wakifanya kazi yao kupinga mambo yale yale ambayo Bwana anawaongoza watumishi wake kufanya. Lakini wakati umewadia kwa wanaume na wanawake kufikiri kwa kulinganisha chanzo cha jambo na matokeo yake. Tumechelewa mno, tumechelewa mno kuanzisha mashirika makubwa ya biashara mijini ----- tumechelewa mno kuwaita vijana wetu wa kiume na wa kike watoke vijijini kuja mjini. Hali zinaendelea kujitokeza mijini zitakazofanya iwe vigumu sana kwa wale wa imani yetu kuendelea kubaki humo. Kwa hiyo, lingekuwa kosa kubwa sana kuweka fedha zetu katika ujenzi wa shughuli za kibiashara mijini. ----- Manuscript 76, 1905.

## Kuishughulikia Miji Kutoka Katika Vituo Vya Mbali

Kwa kadiri inavyowezekana, taasisi zetu zingejengwa mbali na miji. Hatuna budi kuwa na watenda kazi kwa taasisi hizo, na iwapo zinajengwa mjini, hiyo humaanisha kwamba watu wetu hawana budi kukaa karibu nazo. Lakini si mapenzi ya Mungu kwamba watu wake wakae mijini ambamo mna ghasia nyingi [makelele] na machafuko. Watoto wao na waepushwe na hali hiyo; maana mfumo mzima wa mwili huathirika kitabia kwa ghasia za kwenda huku na huko, kukimbia-kimbia ovyo na makelele. Bwana anawataka watu wake wahamie kule shamba [vijijini], ambako watakaa kwenye mashamba yao, na kupanda matunda yao pamoja na mboga za majani, tena, mahali pale watoto wao wanapoweza kuangalia moja kwa moja kazi za Mungu katika maumbile [viumbe vya asili]. Nendeni na familia zenu mbali na miji ndio ujumbe wangu.

Kweli ni lazima isemwe, haidhuru kama watu wataisikia [wataizingatia], au wataikataa. Miji imejaa majaribu mengi. Tungepanga mipango yetu ya kazi, kwa kadiri iwezekanavyo, kwa namna ambayo tutaweza kuwazuia vijana wetu wakubwa mbali na uchafu huo.

Miji inatakiwa kushughulikiwa kutokea kwenye vituo vya mbali. Akasema yule mjumbe wa Mungu, "Je! hivi miji hiyo haitapewa onyo? Naam; si kwa njia ya watu wa Mungu kuishi humo, bali kwa njia ya wao kuitembelea, na kuwaonya juu ya kile kinachokuja juu ya ulimwengu huu." ----- Letter 182, 1902.

## Mahali Pale Ambapo Ni Rahisi Kuifikia Miji Hiyo

Hebu watu wenye akili timamu wachaguliwe, sio kwa kusudi la kutangaza kile wanachokusudia kufanya, bali kwa ajili ya kutafuta mali ya kumiliki katika maeneo yale yaliyo katika wilaya za vijijini, mahali pale ambapo ni rahisi kuifikia miji hiyo, panapofaa kujenga shule yetu ya mafunzo kwa ajili ya watenda kazi wetu, mahali ambapo panaweza kujengwa huduma za kuwatibu watu na kuwahudumia wale wasioijua kweli. Tafuteni mahali kama hapo nje tu ya miji mikubwa, mahali ambapo majengo yanayofaa yanaweza kupatikana, aidha kama zawadi toka kwa wenye majengo hayo, au kwa kuyanunua kwa bei nzuri kutokana na misaada ya fedha iliyotolewa kwa hiari toka kwa watu wetu. Msijenge majengo katika miji hiyo iliyojaa makelele mengi. ----- Medical Ministry, uk. 308,309. (1909).

## Mafundisho Toka Kwa Henoko na Lutu

Sisi kama watu wake Mungu wanaozishika amri zake [kumi] ni lazima kuihama miji. Kama vile alivyofanya Henoko, hatuna budi kufanya kazi yetu [ya kuongoa roho] mijini, lakini tusikae humo. ----- Evangelism, uk. 78,79. (1899)

Maovu yanapozidi sana katika taifa lo lote lile, daima husikika sauti fulani inayotoa onyo na mafundisho, kama vile sauti ya Lutu ilivyosikika kule Sodoma. Hata hivyo, Lutu angeweza kuiokoa familia yake kutokana na maovu yale mengi, kama asingalikuwa amefanya makazi yake katika mji ule mwovu, ambao ulikuwa umejaa uchafu mwingi. Mambo yote ambayo Lutu na familia yake walifanya mle Sodoma wangeweza kuyafanya hata kama wangeishi mahali fulani mbali kidogo na mji ule. Henoko alitembea na Mungu, lakini hakukaa katikati ya mji wo wote uliochafuka kutokana na kila namna ya vitendo vya kikatili vya kutumia nguvu pamoja na uovu, kama Lutu alivyofanya kule Sodoma. ----- Evangelism, uk. 79. (1903)

## Makanisa, Ila Sio Taasisi, Kuwamo Mijini

Tena na tena Bwana ametuagiza sisi kuwa inatupasa kuishughulikia miji kutokea kwenye vituo vyetu vilivyo mbali. Katika miji hiyo hatuna budi kuwa na nyumba zetu za ibada [makanisa], kama kumbukumbu za Bwana, lakini taasisi za kuchapisha vitabu vyetu, za kuponya wagonjwa, na zile za kuwafundisha watenda kazi wetu; zinapaswa kujengwa nje ya miji. Hasa ni muhimu kwamba vijana wetu waepushwe na majaribu ya maisha ya mjini.

Inapatana na agizo hilo, kwamba nyumba za kukutania [makanisa] zimenunuliwa na kuwekwa wakf katika mji wa Washington na Nashville, ambapo nyumba za uchapishaji na hospitali zilizo katika vituo hivyo zimejengwa mbali na sehemu za katikati za miji hiyo yenye msongamano wa watu wengi sana, kama vituo vya kazi vilivyo mbali na mji. Huo ndio mpango uliofuatwa katika kuziondoa nyumba nyingine za uchapishaji pamoja na hospitali na kuzijenga mashambani [vijijini], na jambo hilo linafuatwa kule Uingereza kwa habari ya nyumba ya uchapishaji ya London pamoja na shule ya mafunzo iliyopo pale. Hivi sasa tumepewa nafasi ya kusonga mbele kwa maongozi ya Mungu yaliyofunuliwa kwa njia ya kuwasaidia ndugu zetu katika vituo hivyo muhimu na vinginevyo kwa kuanzisha kazi yetu juu ya msingi ulio imara, ili ipate kuendelezwa mbele kwa uthabiti. ----- Special Testimonies, Series B, No. 8, uk. 7,8. (1907)

Tunatakiwa kuwa na busara kama nyoka na wapole kama hua katika juhudi zetu za kutafuta mali ya kumiliki kule shamba [vijijini] kwa bei ya chini, na kutoka kwenye vituo hivyo vya mbali tunapaswa kuihudumia miji hiyo. ----- Special Testimonies, Series B, No. 14, uk. 7. (1902)

## Ujumbe Tuliopewa na Bwana

"Tokeni mijini; tokeni mijini!" ----- huo ndio ujumbe alionipa Bwana. Matetemeko ya nchi yanakuja; mafuriko yanakuja; sisi hatutakiwi kujijenga katika miji hiyo miovu, ambamo yule adui [Shetani] anatumikiwa kwa kila njia, na ambamo Mungu mara nyingi anasahauliwa. Mungu

anataka tuwe na macho safi ya kiroho. Yatupasa kuwa wepesi kutambua hatari kubwa ambayo ingeweza kuambatana na ujenzi wa taasisi zetu katika miji hiyo miovu. Yatupasa kupanga mipango yetu kwa busara ili kuionya miji hiyo, na wakati uo huo kuishi mahali pale tunapoweza kuwakinga watoto wetu pamoja na sisi wenyewe dhidi ya mivuto ile michafu inayoharibu tabia ambayo imeenea sana mahali hapo. ----- Life Sketches, uk. 409, 410. (1906)

## SEHEMU YA TISA

## Kukimbia Wakati wa Hatari Mwishoni mwa Pambano Hilo

### Ishara ya Kuanza Kukimbia

Huu sasa sio wakati kwa watu wa Mungu kuendelea kuyakaza mapenzi yao au kujilimbikizia hazina zao katika ulimwengu huu. Wakati hauko mbali, ambapo sisi, kama wanafunzi wale wa mwanzo [wa Yesu], tutalazimika kutafuta kimbilio letu maporini na mahali pasipo na watu. Kama vile kule kuzingirwa kwa Yerusalemu na majeshi ya Warumi ilivyokuwa ishara ya kukimbia kwa Wakristo wale wa Yudea, hivyo ndivyo, kule kujitwalia madaraka kwa upande wa taifa letu [la Marekani] kwa njia ya kutunga amri ile inayowalazimisha watu wote kuitunza sabato ya papa [Jumapili], kutakavyokuwa onyo kwetu sisi. Wakati huo ndipo saa itafika ya kuondoka katika miji mikubwa, tukijiandaa kuihama miji midogo ili kwenda mafichoni kwenye makazi yale ya upweke katika milima. Na, kwa sasa, badala ya kutafuta hapa [duniani] makazi yaliyojengwa kwa gharama kubwa, tungekuwa tunajiandaa kuhamia kwenye nchi ile iliyo bora, yaani, ile ya mbinguni. Badala ya kutumia fedha zetu kwa kujifurahisha nafsi zetu, tungekuwa tunajifunza kubana matumizi [kutumia fedha zetu kwa uangalifu sana]. ----- Testimonies, Gombo la 5, uk. 464,465. (1885)

JIPATIE VITABU HIVI VIPYA KABISA!

Vitabu vipya kadhaa vimekwisha kuchapishwa na vingine vimo mbioni kuchapishwa. Wasomaji wanaotaka kujua habari zaidi pamoja na bei za vitabu hivyo wanaombwa kuandika barua zao kwa Leaves of Life International, P.O. Box 17, MAFINGA, Tanzania:-

1. KRISTO NA HAKI YETU, na E. J. Waggoner.

Kitabu hiki ni muhimu kwa kila Mkristo anayetaka wokovu ili awe tayari kumlaki Yesu hewani.

2. UPONYAJI WA MUNGU, na Mary Ann McNeilus, M.D.

Kitabu hiki ni muhimu kuwa nacho. Punguza gharama za matibabu kwa kutumia njia 8 rahisi ambazo hazigharimu fedha. Epukana na magonjwa yasiyokuwa ya lazima. Jifunze matumizi ya maji na mkaa kwa tiba rahisi za kushangaza.

3. MWITO WETU MKUU, na E. G. White.

Kitabu cha kesha la asubuhi kwa mwaka mzima. Kila robo mwaka ina kijitabu chake. Robo nne hufanya kitabu kizima cha kudumu. Usizitupe. Tunza kwa matumizi ya kila mwaka.

4. MNYAMA, JOKA, NA MWANAMKE, na Joe Crews.

Unabii unaolinganisha Pembe Ndogo ya Danieli 7 na Mnyama kama Chui wa Ufunuo 13. Ni nani huyo? Ana athari gani kwako na kwa ulimwengu mzima? Usikikose kujipatia kitabu hicho.

5. TOKA SABATO KWENDA JUMAPILI, na Carlyle B. Haynes.

Kitabu ulichokuwa ukikihitaji ili kujibu hoja zako zote juu ya Sabato na Jumapili. Mabadiliko ya kalenda, sabato za kivuli, na kadhalika. Utunzaji wa Jumapili ulivyoanza pamoja na semi mbalimbali za Viongozi wa Kiprotestanti juu ya Sabato.

6. UGONJWA NA SABABU YAKE, na E. G. White.

Kwa nini wanadamu wamedhoofika na wanazidi kudhoofika hivyo? Kwa nini ni vibaya sana kuoana watu waliopitana umri kwa miaka mingi sana? Kuna madhara gani? Kwa nini madawa ya kisasa ambayo ni sumu sio suluhisho kwa tiba halisi ya mwili? Usikose kujipatia kitabu hiki.

7. IMANI NA MATENDO, na E. G. White.

Wengi wamechanganyikiwa kuhusu fundisho hilo la imani na matendo. Na wengi watapoteza wokovu wao kwa kutokuwa na hakika juu ya mambo hayo mawili.

8. SIKU YA BWANA, na R. J. Wieland.

Kuna utata mkubwa kuhusu Siku ya Bwana miongoni mwa Wakristo. Wengine wanadhani ni Jumapili, na wengine wanadhani ni Jumamosi. Biblia yasemaje? Mwandishi huyu amelifafanua suala hili kwa njia rahisi kabisa.

9. MSALABA NA KIVULI CHAKE, na Stephen N. Haskell.

Somo la Patakatifu limeelezwa kwa njia rahisi sana inayoeleweka kwa mtu wa kawaida. Huduma ya hekalu la duniani ilikuwaje? Huduma ya hekalu la mbinguni ikoje? Wokovu wako unaathiriwaje na huduma ile ya mbinguni? Yesu anafanya nini sasa mbinguni? Maswali hayo yanajibiwa. Sabato 7 za kivuli zaWakolosai 2:16,17 zimefafanuliwa humo.

10. HATARI KUBWA MBELE YETU, na Robert W. Olsen.

Matukio ya kutisha ya siku za mwisho yameelezwa waziwazi humo. Usikose kukinunua.

VITABU ZAIDI VINAANDALIWA KWA AJILI YAKO.